SWAHILI FORUM 11 (2004): 211-226

CHACHAGE SEITHY L. CHACHAGE: *MAKUADI WA SOKO HURIA* (2002)[1]. UCHAMBUZI NA UHAKIKI

JOHN P. MBONDE

1. Utangulizi

Chachage Seithy L. Chachage amepata kuandika riwaya nyingine tatu: *Sudi ya Yohana* (1980), *Kivuli* (1984) na *Almasi za Bandia* (1990).[2] Riwaya yake ya nne *Makuadi wa Soko Huria* (2002) ni ya kihistoria na yenye upekee wa maudhui, muundo na mtindo. Vipengele hivi vinadhihirisha ukomavu na upeo wa juu wa mwandishi ilimradi kwenda sambamba na changamoto ya utandawazi ya karne ya ishirini na moja ya milenia ya tatu. Mwandishi amekitabaruku kitabu hiki kwa kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (1922-1999).

2. Muhtasari

Riwaya imegawanyika katika sura kamili kumi na mbili zikitanguliwa na sura iitwayo *Kifungua Pazia* na kuhitimishwa na *Kifunga Pazia.* Kwa maneno mengine tungeweza kusema kuwa kuna jumla ya sura kumi na nne.

Makuadi wa Soko Huria ni hadithi ya kihistoria yenye ukweli unaodhihirika leo. Inatoa taswira ya mapambano ya Watanzania katika kujipatia uhuru na amani ya kweli: mapambano dhidi ya ukoloni na baadaye dhidi ya baadhi ya watu wao walioteka nyara uhuru wa wengi na kushirikiana na wageni kupora rasilimali ya nchi kwa kisingizio cha soko huria.

Hadithi inaweka bayana uozo na udhalimu uliojificha katika mfumo wa soko huria: tamaa ya pesa na nguvu za kiuchumi, ubinafsi na ukandamizaji. Pia ni hadithi ya matumaini. Inatuonyesha jinsi watu wasivyokubali kukandamizwa, wasivyokata tamaa. *Makuadi wa Soko Huria* inatukumbusha kwamba utu wa binadamu hauvunjwi kwa pesa wala kwa mabavu.

Riwaya hii ni riwaya ndugu na ile ya Gabriel Ruhumbika iitwayo *Miradi Bubu ya Wazalendo* (1992)[3] kwa maudhui, muundo na mtindo kwa upande moja, na kwa jinsi wahusika na mtiririko wa matukio na vipengele vingine vya fani vilivyoshonana kwa umahiri wa hali ya juu; ingawa

---

[1] Chachage Seithy L. Chachage. 2002. *Makuadi wa Soko Huria.* Dar es Salaam: E & D Publishers Limited. 287 pp. ISBN 9987 622 45 3.

[2] Chachage Seithy L. Chachage. 1981 [1980]. *Sudi ya Yohana.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press. 101 pp.; Chachage Seithy L. Chachage. [bila mwaka kutajwa] [1984]. *Kivuli.* Dar es Salaam: B.C.I. Publishers. 117 pp.; Chachage Seithy L. Chachage. 1991 [1990]. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press. 115 pp.

[3] Gabriel Ruhumbika. 1992 [^{2}1995]. Miradi Bubu ya Wazalendo. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House. 166 pp.

vipindi vya matukio ya kihistoria kila mmojawao amechukua vyake. Riwaya ndugu hizi zinaakisi na kugusa sana maisha ya jamii nchini Tanzania mijini na vijijini.

Makuadi wa Soko Huria ni riwaya inayochambua na kupembua mfumo wa kisiasa na kiuchumi na mustakabali wa taifa la Tanzania. Wahusika Japhet Lupocho na Mwenerumango wanawakilisha makuadi na wasaliti wengine ambao wameuponda uzalendo wao na kuwa vibaraka wa wawekezaji au wabia. Ndio chui waliovaa ngozi za kondoo – wakoloni mamboleo waliojigubika na wingu la soko huria na utandawazi, kama vile akina Paul Mooney na Balfour Beatty kutoka nchi za nje, na vitimbakwira ambao ni Watanzania wenye dhamana ainaina za uongozi ambao huuza ardhi kwa wafanyabiashara wa mijini na kuwakandamiza wanavijiji wa sehemu husika. Mikataba baina ya nchi na wawekezaji hao yenye mizizi ya ukoloni mamboleo huifanya nchi kutawaliwa kiuchumi. Huo ni mfumo dume wa ukoloni mamboleo ambao ni mgumu sana kung'olewa.

Mhusika Mbunge Luhala bila aibu anampigia debe Mooney ilimradi yeye aweze kumegewa keki ya soko huria ndivyo alivyojidhihirisha kuwa naye ni miongoni mwa makuadi badala ya kuwapigia debe wananchi wanyonge. Mbunge Luhala ni mwakilishi wa viongozi wa ngazi ya juu wanaowakandamiza wananchi na kuwapora haki zao kwa kuwa na miradi kama ule wa ufugaji wa kamba katika bonde la Rufiji, ambao haukuwa na budi kumilikiwa na kuendeshwa na Wanarufiji wenyewe.

Kwa upande mwingine, mwandishi anamtumia mhusika Binti Wenga ambaye siyo *First Lady* wala siyo mtu mashuhuri kisiasa, kuwa ni kichokoo shupavu cha nafasi ya mwanamke katika jamii. Mama huyo hana ubinafsi bali anatumia uwezo wake katika kutetea haki za nchi yake. Hata hivyo mashujaa wanaojiri katika riwaya hii ni wananchi wa kawaida wenyewe, yaani wazee wa Delta ya Rufiji. (Na tunaweza kuchukulia kwamba katika riwaya hii, Delta ya Rufiji inawakilisha pembe zote za Tanzania zilizosheheni utajiri wa asili.) Wazee hao ni pamoja na akina Miraji na Mrisho. Siasa ya wakazi wa Rufiji haitokani na elimu ya darasani au chuo kikuu, bali ni hekima na busara zao, na upeo wao uliokua na kuendelea kukua kwa kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi na mang'amuzi ya kutoka karne hadi karne na kuwa ndio kiini cha utamaduni wao.

Mhusika Janga Mjuba ni mwandishi na mwanaharakati ambaye pamoja na wenzake wanafadhiliwa na wahisani, wanafunga safari hadi Delta ya Rufiji kuchunguza mradi wa ufugaji kamba kwa ajili ya Bwana Paul Mooney, mwekezaji mashuhuri wa mradi huo. Huko akina Mjuba wanakutana na tajiri-uchwara, Japhet Lupocho, ambaye baada ya kuwa kuadi kwa Mooney anaporwa hekima na busara yake na kumwachia bepari Mooney kuwa na kauli na uamuzi wa mwisho.

Kwa maneno mengine, watakaosoma riwaya hii, watajiona wako uchi katika kioo cha makuadi. Hao hawana budi kujisalimisha, kwani wakazi wa Rufiji kutokana na historia yao ndefu, akina Binti Wenga, mhusika mwingine Amina, na Wazee wakazi wa Rufiji, Mzee Miraji

na Mzee Mrisho, waliomlea Kinjeketile na Bibi Titi Mohamed, mwanamke wa mstari wa mbele katika kupigania uhuru wa Tanganyika, wako mbioni kuwalea akina Janga Mjuba, Sifuni Karanja na Fidelis Mvumi Msakapanofu. Hao watatu tungeweza kuwaita wahusika wakuu. Fidelis Mvumi Msakapanofu ambaye pia ni mwandishi wa habari ni msimulizi anayesimulia hadithi ya riwaya nzima kwa kutumia nafsi ya kwanza.

Mwenzake Janga Mjuba alipata adhabu kubwa kuliko adhabu ile inayotolewa na dola. Mke wake Salama amemnyima haki ya unyumba baada ya kutamka kwamba sasa amekuwa mlokole na mwenendo wa mumewe ulikuwa haufai. Mara kwa mara Janga Mjuba akashamiri katika ulevi ilimradi kupoteza kile wataalam wanachokiita mning'inio wa ziada wa kasumba ya mawazo.

Fauko ya hayo, tunakutana na mwandishi wa habari mwenzake Sifuni, mwanaharakati mwenye msimamo wa kimapinduzi aliyeolewa na Oscar Mayowe. Wakati Oscar alipopelekwa kikazi huko Zanzibar, anamtia mimba binti wa Waziri. Oscar akabadili dini na kuitwa Hassan ili afunge ndoa na binti waziri. Hivyo akauvunja uhusiano wake na mkewe Sifuni.

Hapa tunashuhudia kuwa Mjuba na Sifuni wote wakawa wapweke. Hali hiyo pia huwakilisha ombwe kubwa lilioje miongoni mwa jamii ya wananchi katika vita vya kujikomboa kisiasa na kiuchumi katika mapambazuko na athari za soko huria na utandawazi.

3. Dhamira

Katika sehemu hii tutachambua dhamira zinazojitokeza zaidi katika riwaya hii:

1. Dhuluma na Hujuma
2. Siasa na Uchumi
3. Uongozi
4. Rushwa na Utapeli
5. Ukale na Usasa
6. Nafasi ya Mwanamke katika Jamii
7. Mapenzi na Ndoa
8. Dini
9. Vyombo vya Habari na Utandawazi
10. Maliasili na Mazingira

Kuna dhamira nyingine nyingi ambazo zimejitokeza katika riwaya hii ambazo kwa namna moja au nyingine zinazizunguka hizi zilizoorodheshwa hapa juu.

3.1. Dhuluma na Hujuma

Kwa kweli hii ni dhamira kuu katika riwaya hii. Kuna matukio mengi ya dhuluma na hujuma ambayo yamewekwa bayana na mwandishi katika hadithi hii. Kwa mfano tunaweza kuona jinsi wanavijiji wa Delta ya Rufiji, hususan wa kijiji cha Nyamisati, walivyodhulumiwa:

> *[...] miaka ya sabini, wananchi waliweza kununua mapande ya barafu kwa ajili ya kuhifadhi samaki wao wa kila aina pale kiwandani. Kadhalika kiwanda kilinunua samaki wao bila ya matatizo. Mwanzoni mwa miaka ya themanini ndipo matatizo yalipoanza kutokea kiwanda kilipoanza kukopa kwa wavuvi badala ya kuwalipa fedha taslimu, na mabarafu yakaanza kukosekana, ingawa mabosi wa kiwanda*

> *walinawiri. Hatimaye kilikabidhiwa kwa kukodishwa kwa Bwana Vangalatus, Mgiriki [...] alidai kwamba angesaidia wananchi, lakini akaishia kuwakopa wavuvi na kuwalipa pesa kidogo kuliko hata serikali ilivyokuwa ikifanya. Wavuvi wakazidi kufukarika.* (Chachage 2002: 153-154)

Wakati mwingine, hujuma katika vijiji vilivyostawi hufanywa na uongozi wa vijiji hivyo kwa kushirikiana na uongozi wa kata, tarafa, wilaya, mkoa na taifa kwa visingizio vya kila aina.

> *[...] na kila uongozi huo ukija, kijiji kililazimishwa kuandaa sherehe na chakula kwa madai kwamba utamaduni wa Mwafrika ni ukarimu kila mgeni ajapo japokuwa hao viongozi walikuwa wakilipwa masurufu na Serikali.* (ibid.: 108)

Kwa yamkini, wavuvi hao wanaohujumiwa na kudhulumiwa wanawakilisha tabaka la wanyonge na walalahoi wakiwemo wakulima, wafanyabiashara ndogondogo (maarufu kwa jina la Wamachinga), na wengineo.

3.2. Siasa na Uchumi

Siasa na uchumi hutegemeana katika mfumo wa maisha ya kila siku ya jamii. Katika riwaya hii tunasimuliwa historia yote ya eneo la Tanzania Bara tangu miaka ya 1840 hadi leo, na jinsi siasa na uchumi hushonana katika kuangalia historia hiyo. Kwa mfano, harakati za siasa iliyoongozwa na Julius K. Nyerere ilivyowawezesha Watanzania kujipatia uhuru kutokana na minyororo ya kisiasa ya wakoloni, Waarabu, Wajerumani na Waingereza, zinasawiriwa na kujadiliwa katika riwaya hii.

Baadhi ya wanataaluma hasa wale kutoka nje ya nchi walikuwa na mtazamo tofauti juu ya itikadi iliyoanzishwa kwa kuzingatia Azimio la Arusha. Mhusika Paul Mooney aliyekuwa mwalimu katika miaka ya sabini (na kuishia kuwa mwekezaji mkuu wa mradi wa kufuga kamba) alikuwa anafundisha

> *[...] kwamba tatizo la Tanzania lilikuwa ni kupapukia Ujamaa mapema mno, kwani kufuatana na mafuzo ya mwanafalsafa Karl Marx, ilibidi Tanzania na nchi zingine ambazo hazijaendelea kusubiri ubepari ujikite vya kutosha, kwa kuwasaidia mabepari wazalendo, ndipo baada ya hapo ingewezekana Ujamaa madhubuti kujengeka.* (ibid.: 91)

Pahala pengine mhusika Alibhai, Mtanzania wa asili ya Kiasia anaropoka na kusema:

> *"Na hapo ndipo baadhi yetu tulipotofautiana na yule kichwamaji Julius Nyerere, ambaye alitaka kujenga ujamaa kwa misingi ya umaskini. Huyu Shivji aliandika kitabu kilichotudhalilisha baadhi yetu wenye asili ya Kiasia. Hicho kitabu chake, 'Class Struggle in Tanzania' kilikuwa kinadai kwamba sisi Waasia ni vibwanyente uchwara wa kibiashara; kwamba sisi tulikuwa makuadi wa wanyonyaji wenye mitaji mikubwa kutoka nje."* (ibid.: 120)

Hali kadhalika, tunasawiriwa mfumuko wa vyama vingi vya kisiasa vikiwa na sera na itikadi mbalimbali, ilimradi kuimarisha demokrasia. Mabadiliko ya kisiasa yanaonyeshwa kwa kusawiri

hamasa ya wananchi ya kuwa na moyo wa kizalendo na kusimama kidete kulinda ardhi, maliasili na kutetea haki zao.

Dhamira ya uchumi imejitokeza mara nyingi toka mwanzo wa riwaya hadi mwisho. Mathalani tunaelezwa jinsi akina Mama N'tilie anavyojituma ilimradi aweze kuyakimu maisha yake (tz. ibid.: 101). Pia, tunaelezwa kuhusu shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wananchi wa Rufiji ikiwa ni pamoja na uvuvi, ukataji na uuzaji wa mikoko. Hali kadhalika, tunasimuliwa mgogoro baina wanavijiji wa Ruhimba kuhusu kupendekeza kilimo cha tumbaku kama zao la kibiashara au kilimo cha mazao ya chakula.

> *[...] serikali ilivyoviingilia hivi vijiji* [vilivyojitegemea] *na kuvivunja kwa kuonekana kuwa tishio kubwa kwa serikali, hasa baada ya wanavijiji hawa kukataa kulima tumbaku, wakidai kwamba kwao ilikuwa faida kubwa zaidi kulima* [mazao ya] *chakula. Hii iliwaudhi sana wanasiasa na hasa Mkuu wa Mkoa Bwana Edward Barongo [...]* (ibid.: 107)

3.3. Uongozi

Dhamira hii ina sura mbili: uongozi bora na uongozi mbaya. Sura zote mbili zimejitokea katika riwaya hii. Kwa mfano, mwenyekiti wa kijiji cha Nyamisati, Bwana Nyakilanzi, ni kiongozi bora kwani anawashirikisha wanakijiji wake katika kufanya maamuzi na kupanga mipango na kuitekeleza kwa maslahi ya umma. Anakuwa mstari wa mbele katika majukumu yote pale kijijini. Hana ubinafsi, na kwa misingi hii huwa ni mtu wa watu.

Kwa upande mwingine, tunamwona Japhet Lupocho alivyo na uroho wa pesa na kuhodhi maslahi mengi kwa faida yake binafsi. Huyu anawakilisha uongozi mbaya. Pia tunaambiwa na Nyakilanzi jinsi viongozi wa ngazi ya juu wasivyowajali watu.

Katika sura ya saba Nyakilanzi analalamika dhidi ya uongozi mbaya:

> *[...] walikuwa wamefikiwa na ugeni wa Makamu wa Rais asubuhi hiyo [...] "Wanataka kufuga kamba! [...] Tunasikia kwamba wanataka kuchimba mahandaki Rufiji yote na kutuhamisha tukaishi kwingine. Tukaishi wapi? Hawa wamekusudia kuangamiza maisha yetu na kututokomeza tupotee kabisa katika uso wa dunia hii! [...] Naye Makamu wa Rais alifika hapa na kihelikopta chake [...]"* (ibid.: 152)

Halafu, Nyakilanzi anaongezea kwa masikitiko dhidi ya hotuba ya Makamu wa Rais:

> *"Haikuwa hotuba, bali matusi kwa kadri tunavyofahamu sisi. Alidai kwamba sisi watu wa Rufiji ni wavivu na ndiyo maana hatuna maendeleo. Alidai kwamba raslimali tunazo lakini tumezikalia, na kutokana na tabia zetu za ushirikina, sasa tunapinga uwezekano wa kuwepo mradi [...] ndiyo sababu tulikuwa tunaishi kwenye madungu na kushindwa hata kuwanunulia wake zetu nguo za ndani! [...] Na hao wabunge wetu walitikisa vichwa kwa kuitikia pale mbele, kama vile sisi hatukuwachagua!"* (ibid.: 152)

Mfano mwingine wa uongozi mbaya tunaukuta katika mawazo ya Binti Wenga:

> *Ala! Kumbe huyu ni Mheshimiwa Luhala! Mwaka 1990 alikuwa mwembamba, hakuwa hivi hata kidogo, ndiyo maana alikuwa amemsahau! Tangu alipokuja kufanya kampeni zake mwaka ule na kuchaguliwa, alikuwa hajafika tena hapa kijijini. [...] Binti Wenga [...] alikuwa akiyafikiria mambo yaliyokipata hiki kijiji katika historia yake [...]: ile miradi ya maji, mashine ya kukobolea na kusagia, trekta, duka la kijiji pamoja na la akina mama, shamba la ushirika na hata zahanati na shule vilikuwa vimekufa. Uongozi wa kijiji ulikuwa umevifilisi vyote."* (ibid.: 113-114)

Binti Wenga alikerwa sana na uongozi mbaya wa Mbunge:

> *Huyu mbunge mbele yake, alikuwa hajakanyaga hapa kijijini hata mara moja toka apate kura zake, na leo alikuwa amerudi kwa kusudi hilohilo!* (ibid.: 114)

3.4. Rushwa na Utapeli

Katika riwaya tunaonyeshwa jinsi wawekezaji walivyoshamiri katika utoaji wa rushwa kwa vigogo serikalini na kwa vikaragosi vyao ili wawapigie debe. Mmoja kati ya wawekezaji hao ni Mwingereza Paul Mooney (na tunaweza kuchukulia kwamba jina lake linadokeza maana ya 'Bwana Pesa'). Alitoa rushwa na kuwarubuni vigogo na wanyonge wa Delta ya Rufiji, Mererani na hata katika mkutano uliofanyika katika Ukumbi wa Utamaduni wa Korea ambao uliwahusisha wapokea rushwa (posho) wakiwemo wanasiasa, watendaji wa wizara mbalimbali, ujumbe wa watu kutoka Rufiji na mpigadebe wake Japhet Lupocho. Wajumbe wa Baraza la Mazingira kutoka Rufiji wanamwandama Lupocho:

> *"Kwanza wewe umeletwa na nani hapa kwenye mkutano? [...] Wewe na wenzako mliokuja hapa kutetea mradi mmeletwa na mwekezaji. Mmehongwa nyie!"* (ibid.: 23)

Mwalimu Lipuka, Mkuu wa shule ya msingi ya Ruhimba bila aibu anadhihirisha kutekwa nyara na Mbunge na mwenyekiti Matola katika mizengwe ya upokeaji rushwa na kuthubutu kumghilibu Binti Wenga na kusema bila aibu:

> *"Mama, mbunge wetu ametoa shilingi laki mbili leo asubuhi kwa ajili ya kutengeneza madawati ya shule ili watoto wetu wasome kwa raha."* (ibid.: 114)

Mhusika Mjuba anayewapigania haki wananchi wa hali ya chini anasongwa na msitu wa mawazo:

> *[...] kuhusu utoaji wa rushwa kwa ajili ya kununulia kura, hayo magari na raslimali zilizotumika kwa ajili ya ushindani wa kisiasa: barabara ngapi au zahanati ngapi au vitabu vingapi vingeweza kununuliwa kwa raslimali zote hizo zilizotumika kuwaleta watu huku bungeni ambako waliutumia muda wote kwa maslahi yao kuliko kile kilichowatuma? Tulikuwa tumewatuma huku waje kutudhihaki sisi wenyewe tuliowachagua?* (ibid.: 276)

Katika muktadha mwingine, tunaonyeshwa utapeli unaojidhihirisha katika baadhi ya taasisi zisizo za kiserikali [*NGOs*] zikiongozwa na Wazungu.

> *[...] hawa Wataliano [...] wakilichukulia hili suala la wakimbizi na mradi wa kujikimu maisha yao. Kazi yao kubwa ilikuwa kutafuta hela za msaada na wakifanya hivyo walikuwa hata wakitoa idadi ya uongo na matatizo ya uongo ya wakimbizi. Licha ya hivyo, asilimia themanini ya fedha za msaada zilizoletwa, kama alivyogundua baada ya kufanya nao kazi kwa miaka minne, zilikuwa zikiishia mifukoni mwao.* (ibid.: 185)

3.5. Ukale na Usasa

Kuhusu mambo ya kale, tunaelezwa juu ya historia ya wakati wa ukoloni. Wananchi wengi walijiandikisha manamba ama kwenda pwani kukata mkonge au kwenda Afrika Kusini kwenye migodi. Baba mkubwa wa Binti Wenga alikwenda Afrika Kusini. Kwanza akafanya kazi ya uboi kwa Wazungu, na baadaye akaajiriwa kama kibarua katika kampuni ya uvuvi ya *Donkerkirt*. Aliporejea kutoka Afrika Kusini daima alipenda kuwasimulia watu juu ya vituko vilivyowasibu wakati akiwa kwenye kampuni hiyo, na hivyo pale kijijini wakampachika jina la 'Donkrakiti' (tz. ibid.: 37). Kwa maneno mengine, hao manamba waliobahatika kurejea makwao walikuja na tamaduni za huko yakiwemo majina waliojipachika, mavazi, lugha na wengine walirejea na wake waliowaoa huko.

Tunaelezwa pia juu ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia na jinsi askari wa Kijerumani walivyopambana na askari wa Kiingereza waliokuwa katika meli zilizoitwa *Königsberg* na *City of Winchester* na kuiteka nyara pamoja na shehena ya chai kutoka India, na jinsi vilivyoleta athari ya uchafuzi wa mazingira, samaki kufa ovyo na kuelea juu ya maji, na papo hapo wananchi wa vijiji vya Delta ya Rufiji na makandokando yake kusumishwa kutokana na hilo.

Katika enzi ya Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, tunaelezwa vuta nikuvute iliyokuwa inatokea baina ya wanachuo na wazee wa chuo. Wanachuo wanasemekana kuwa wanaota ndoto za kitoto, na wakati huohuo wanachuo walidai haki zao na kuwaelezea wazee kuwa ni utoto wa wakubwa kung'ang'ania mambo yao ya kale ambayo tayari yamepitwa na wakati.

> [Mhusika Mooney:] *"Huyo Profesa* [Shivji] *alipewa hiyo kazi* [kuongoza Tume ya Ardhi] *kama njia ya kumwondoa pale Chuo Kikuu kwa muda fulani ili mambo yatulie kidogo, baada ya kukifunga kutokana na fujo zilizokuwa zimetokea pale hadi kusababisha Rais Mwinyi kutukanwa matusi ya nguoni. Wanasema Rais Mwinyi hakutegemea kwamba huyo Profesa angeweza kufanya hiyo kazi. Hata hivyo, ukweli ni kwamba hakuna Rais ambaye amewahi kufuata maoni ya tume yoyote ile duniani."* (ibid.: 121)

Tunashuhudia pia suala la ukale na usasa linavyoibuliwa mintarafu sera na itikadi za kisiasa.

> [Mhusika Alhaji Said:] *"Dunia imebadilika sana. Hakuna mambo ya ubeberu na ubepari tena enzi hizi. Sasa tunaishi katika mfumo wa duania ya utandawazi ambao unatawaliwa na masoko huria yasiyoepukika hata kidogo. Sahau kabisa ndoto za Nyerere na kifimbo chake."* (ibid.: 18)

Na mhusika Mooney kwa mtazamo wake anabainisha hali tofauti za zamani na sasa:

> *"Soko huria na mfumo wa dunia wa utandawazi ndio umezaa matunda haya. Haya mambo yasingefikirika wakati ule wa ujamaa! Angalau leo tunaona dalili za maendeleo."* (ibid.: 87)

3.6. Nafasi ya Mwanamke Katika Jamii

Vitendo vya kuwadhalilisha wanawake miongoni mwa jamii nyingi duniani bado linatawala sana. Licha ya kunyanyaswa, kuonewa, kudhulumiwa na kuhujumiwa, wanawake wengi hunyimwa haki zao. Mwandishi amewaainisha wanawake katika makundi mawili, yaani wale ambao ni mfano wa kuigwa na wale ambao ni kikwazo kwao wao wenyewe, kwa wanawake wenzao na hata kwa jamii nzima.

Wanawake wa kijiji cha Ruhimba walinyimwa haki zao za kulipwa pesa kuhusu ardhi yao iliyonunuliwa: *[...] waliokuwa wanapewa malipo walikuwa wanaume tu, nyumba zilizokuwa na wanawake peke yao zilinyimwa kwa madai kwamba kimila ardhi ni ya mwanaume* (ibid.: 116). Kutokana na tatizo hili wanawake wa kijiji cha Ruhimba wakachachamaa: *Ni hali hii iliwafanya wanawake wa Ruhimba wamtume Binti Wenga kwenda Dodoma [...]* (ibid.: 116). Huyu mhusika Binti Wenga anasawiriwa kama ni mwanamke ambaye ni mfano wa kuigwa: *Alikuwa ni mwanamke aliyeshuhudia ukombozi mpya, akaheshimiwa na wanawake wote, na kuhofiwa na wanaume wa pale kijijini [...]* (ibid.: 111).

Hata hivyo, katika mkutano wa Paul Mooney uliofanyika katika ukumbi wa utamaduni wa Korea jijini Dar es Salaam tunaona jinsi wanawake wasivyowakilishwa:

> *"Mimi sikumuona hata mwanamke mmoja kutoka Rufiji pale. Hakuna wanawake huko Rufiji?"* (ibid.: 27)

Dhuluma dhidi ya wanawake inasawiriwa kwa kutoa mfano wa mhusika Anna, mkazi wa mjini Dodoma ambaye alitiwa mimba na Mbunge Njovu Luhala hata kabla hajamaliza darasa la saba.

> *Huyo Mbunge alikuwa amemdanganya Anna kwamba angemwoa na kumpeleka akaishi katika nyumba yake huko Mfaranyaki, Songea mjini [...] Lakini toka alipopata mimba na kujifungua hao mapacha, Mbunge Luhala alikuwa akimkwepa kila akija Dodoma.* (ibid.: 44)

Mhusika Sifuni Karanja anawakilisha wanawake waliosoma. Ni mwanahabari na mwenyekiti wa WAMAJA, shirika la waandishi wa habari. Anasawiriwa kama ana nidhamu ya hali ya juu ikiwa ni matunda ya malezi bora na mafunzo ya kijeshi ambayo aliyapata kwenye Jeshi la Kujenga Taifa na kumfanya awe mkakamavu na mwenye msimamo wa kuzingatia maadili yake barabara. Sifuni anayakumbuka maisha ya jeshini na jinsi alivyokuwa jasiri kuusema ukweli dhidi ya Afande Chacha mbele ya Afande Kongoro. *"Mwongo! Mwongo huyu! [...] Alitaka kuni..."* (ibid.: 75). Mkuu wa Kambi alipomtembelea Sifuni akiwa amelazwa katika zahanati, Sifuni alimfichua ukweli wa kujifanya kuugua homa kali (tz. ibid.: 78): Alijiokoa kutoka kwa maafande Chacha na

Kongoro waliojaribu kumbaka. Matokeo yake ni kwamba maafande hao wakafukuzwa katika ajira ya jeshi na kupelekwa kufungwa kwenye gereza la Ukonga na kazi ngumu. Ni dhahiri kwamba Sifuni alikuwa ni mkombozi siyo tu kwa wanawake wengine pale kambini bali hata wavulana kwa matendo ya kikatili kupita kiasi waliyokuwa wanashinikizwa na maafande.

Aidha, msimulizi anawasifu Wanarufiji kwa 'binti' yao maarufu Bibi Titi Mohamed:

> *[...] hawa watu dhalili wa Rufiji ambao walikuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru, hao watu waliokuwa na uzao wa wanawake maarufu na jasiri kama Bibi Titi Mohamed wakati wa kupigania uhuru wa Tanganyika wakaishia kuhainiwa baada ya miaka thelathini na tano ya Uhuru?* (ibid.: 212)

Kushiriki kwa Bibi Titi Mohamed hakukuchangia ukombozi wa akina mama tu, bali kwa kiasi kikubwa kuileta changamoto isiyo na kifani kwa Watanganyika wote, wake kwa waume, kupata mwamko zaidi katika harakati za kupigania uhuru wa nchi yao.

3.7. Mapenzi na Ndoa

Hapa na pale katika riwaya hii kuna vipengele vinavyoweka bayana dhamira ya mapenzi na ndoa. Katika 'Kifungua Pazia' mwanzoni mwa riwaya tunaona jinsi Mjuba na Sifuni wanavyozungumza kwa lugha ya kimapenzi:

> *"Naionea wivu sidiria yako, shimizi yako, chupi yako, hereni zako na nguo zako! Natamani mimi ningekuwa chupi yako!"* (ibid.: 2)

Kuhusu dhamira ya ndoa, tunaelezwa kwamba kuoa wanawake wengi au kuwa na nyumba ndogo limeota mizizi miongoni mwa wanaume wengi barani Afrika.

> *"Karibu wazee wengi pale kijijini walikuwa na wanawake wa pembeni au wa pili na watatu, wasichana wadogo kabisa."* (ibid.: 47)

Hali kadhalika, dhamira hii hujitokeza katika sura nyingine kama inavyokejeli sentensi ifuatayo:

> *"Huko kwa Eliasi ndiko unakofanyia maasi yako ya kimwili?"* (ibid.: 63)

Katika sura ya nne tunaelezwa kwamba Lupocho alimtorosha Amina binti Miraji na kwenda naye hadi Dar es Salaam:

> *Lupocho alipendwa na wanawake wengi sana maishani mwake, na alizaa na baadhi yao, lakini hakuna hata mmoja aliyepata kuishi naye, na wala kujua waliishi wapi. Wazo la kuoa halikuwahi kumjia akilini hata mara moja.* (ibid.: 95)

Aidha, tunaelezwa kwamba Mjuba na Sifuni wakiwa huko Nyamisati walikaa faraghani na kila mmoja kati yao alimtolea siri mwenziwe. Sifuni anamtobolea siri Mjuba:

> *"Si bora wewe miaka mitatu tu. Mimi inakaribia miaka kumi na tano sijui hiyo haki ya unyumba [...] Hebu niambie ukweli, hivi kweli katika miaka mitatu hujatembea nje ya ndoa yako baada ya mambo kuharibika kiasi hicho?"* (ibid.: 207)

Mhusika Mjuba baada ya kulewa pombe alisimulia vituko vya nyumbani kwake na ndoa yake.

> *"Kunyimwa unyumba kwa miaka mitatu na kudhalilishwa kijinsia! Kunyimwa kitendo cha ndoa! Hapo nikasema: hebedari! Inatosha! Kwaheri ewe ndoa laanifu! Na sidhani kama nitarudi tena huko! Bora mara kumi kuanza upya."* (ibid.: 139)

Dhamira hiyo ya ndoa inaonyeshwa kwa mifano mizuri na mibaya. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa ndoa ya Janga Mjuba na mkewe Salama imesambaratika (tz. ibid.: 1). Kwa upande mwingine mhusika Wenga anasimulia umuhimu wa ndoa kwani licha ya kuendeleza koo mbalimbali, ni msingi wa familia, jamii na taifa (tz. ibid.: 37-40). Kwa njia ya ndoa mila na desturi huweza kudumishwa na kuendelezwa katika jamii.

3.8. Dini

Kuhusu dhana ya dini katika riwaya hii, hapa tutazunhumzia vipengele viwili tu.

Kwanza, ni jinsi dhana ya ulokole na wafuasi wanavyoonyeshwa katika riwaya hii. Tunaelezwa kwamba Salama, mkewe Janga Mjuba, amekuwa mlokole baada ya kushiriki katika mahubiri ya kilokole uwanjani pa Jangwani.

> *Na tayari alikuwa amewabatiza watoto majina mengine. Nkrumah aliitwa Bill Graham, jina la mwinjilisti wa kilokole wa Kimarekani aliyeshabikia vita vya Marekani dhidi ya Wavietnam, waliodaiwa kwamba ni Makomunisti wasiomcha Mungu. Bob Marley alipewa jina la Abrahamu yule aliyebarikiwa na Mwenyezi Mungu kuwa chanzo cha taifa teule takatifu la Waisraeli."* (ibid.: 4)

Baadaye tuaona athari za uamuzi huo. Salama anamsuta mumewe:

> *"Bila hata wewe kuzaliwa upya, nadhani maisha yetu ya ndoa hayatakuwa mazuri. Kama hivi leo umekunywa pombe, basi ujue kwamba hakuna haki ya unyumba!"* (ibid.: 33)

Kipengele cha pili ni jinsi dini zilizo rasmi zinavyoshonana na dini za kijadi. Kwa mfano, Janga Mjuba anayakumbuka maneno ya hekima na busara ya babu yake yaliyosimuliwa na bibi yake.

> *"[...] Akawaomba mizimu na miungu kuwa ukue uwe mtu mzima, maisha yako yawe ya heri na fanaka, kisha uige mfano wa ndege mlembe, uwaongoze watu wema na waadilifu kwenye asali, na wazandiki wote na wale watesao roho za watu kwa nyegere, kile kicheche ambacho hurina asali kwa kuwafukuza nyuki kwa ushuzi na kuwashambulia binadamu na wanyama sehemu za viungo vya siri!"* (ibid.: 204)

Katika sehemu nyingine ya matini tunashuhudia tena mshonano huo:

> *[...] walikwenda kwa Maalim ambaye alikuwa mganga ili amsomee dua. Maalim aliwataka walete kuku, mkate wa kumimina, nazi na vifaa vingine vya kumzingulia. Huku akifukiziwa ubani, uvumba na udi na kupewa hirizi, akaombewa kwamba Mwenyezi Mungu amfungulie milango ya heri. [...] Halikuwa dua tu, bali pia alikuwa amepungwa pepo [...]* (ibid.: 257)

3.9. Nafasi ya Vyombo vya Habari na Utandawazi Katika Jamii

Dhamira hii imetawala sana katika riwaya hii toka mwanzo hadi mwisho. Hii inaashiria jinsi vyombo vya habari zinavyoweza kuibua hisia na pia kuchokonoa ukweli wa mambo. Pia wanahabari wanavyofaulu kuigutusha serikali na asasi mbalimbali kuhusu vitimbwi vya uhalifu au ukiukaji sheria unavyozorotesha matarajio ya wananchi. Mfano mzuri wa mwanahabari mwanaharakati ni msimulizi Fidelis Msakapanofu:

> *Hawa wamiliki wa vyombo vya habari wanaojifanya kupenda ukweli, lakini ni wauza habari kama bidhaa nyingine yoyote sokoni walikuwa wameshanichosha!* (ibid.: 13)

Vyombo vya habari vinachukuliwa kuwa ni watetezi wa wanyonge. Mhusika Alhaji Said anasema:

> *"Kama siyo hivi vyombo vya habari vya watu binafsi sasa hivi tungekuwa wapi na vile vimshahara vya njaa vya magazeti ya Chama na Serikali?"* (ibid.: 18)

Umuhimu wa vyombo vya habari katika siasa umesisitizwa sana katika riwaya hii. Kwa kupitia maelezo ya mhusika Paul Mooney tunasoma kwamba

> *[...] hali ya kisiasa ilivyokuwa ikielekea, ilionyesha wazi kwamba vyombo vya habari vingekuwa na jukumu kubwa zaidi katika masuala mbalimbali katika miaka inayokuja kuliko hata nyadhifa za kisiasa.* (ibid.: 92)

Wenye madaraka na mamlaka serikalini au taasisi ziwazo hawapendi wanahabari kwenda kuchunguza na baadaye kuyalipua katika vyombo vyao vya habari.

> *"Mkurugenzi amesisitiza kwamba hamuwezi kuruhusiwa kwenda huko* [Rufiji] *bila kibali chake, na kama ni kuandika habari za huko, kuna waandishi wa habari ambao wameshaandaliwa kusafiri na viongozi hao."* (ibid.: 103)

3.10. Maliasili na Mazingira

Hii ndiyo dhamira iliyokita kina kirefu katika riwaya hii kwa kudokeza mahali mbalimbali nchini kwenye uharibifu wa mazingira.

> *Jumuia ilitaka wanahabari waende wakatembelee Kondoa, ambako matatizo ya mazingira yalishaanza kutangazwa tangu mwaka sabini na moja, baada ya Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, kutembelea huko na kujionea mwenyewe jinsi misitu ilivyokuwa imemalizwa na mmomonyoko kumaliza ardhi.* (ibid.: 21)

Wananchi wa Delta ya Rufiji wanatoa msimamo wao wa kizalendo na haki zao katika mazingira. Mhusika Mzee Abdurrahman anaeleza:

> *[...] "Haya mazingira ya Delta ya Rufiji, huu msitu wa mikoko na mimea ya kila aina iliyomo, hivi visiwa vilivyotapakaa kote, na mengine mengi, ndiyo yametupa daima uhuru wa nafsi, tukaishi kama tutakavyo. Na ndiyo sababu tumekuwa wepesi kuelewa nini maana ya Uhuru kwa miaka yote. Sisi wote wa sehemu hii tunaamini kwamba tu ndugu, na vyote vilivyomo humu ni wakfu. Ni mali ya Mwenyezi Mungu, Wavyale ndio wamekuwa walinzi wa maeneo yote kimila."* (ibid.: 221)

Uvuvi haramu huharibu mazingira kwa viumbe baharini. Yafuatayo ni maelezo ya mhusika Mzee Miraji yaliyosimuliwa:

> *Kuna Mzungu wa kutoka Norway, Bwana Erik Odgaard, ambaye alishakuwa rafiki mkubwa wa wenyeji wa huku kutokana na utetezio wake wa mazingira, ambaye alijaribu kuweleza yule afisa kwamba tatizo siyo wakulima, ambao walikuwa wameshaanza hata kupanda mikoko katika sehemu ambazo walikuwa hawazilimi: tatizo ni serikali yenyewe ambayo ilikuwa imetoa vibali vingi mno vya uvuvi kuliko uwezu wa eneo kuhimili.* (ibid.: 253)

Aidha, mara kwa mara kumejitokeza migongano ya jinsi sera ziletavyo mitanziko.

> *Kilichowashangaza watu wa Rufiji, ni kwamba, ilikuwaje baadhi ya Wazungu wawasaidie katika kutetea sehemu zao na wakati huohuo waje wengine kuwapiga vita hao watetezi? Kwa nini Serikali iwakaribishe Wazungu wa aina mbili kwa wakati mmoja? Halafu, Serikali hiyohiyo isisitize suala la ulinzi wa mazingira na wakati huohuo iwape wageni ruksa ya kuyaharibu?* (ibid.: 254)

Pia dhamira hii inajitokeza katika suala la uchimbaji migodi. Kama inavyosawiriwa, husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na pia huleta athari mbaya kwa watu. Kutokana na kuwa na zana duni katika machimbo, mathalani ya Mererani, wachimbaji wadogo huathirika sana kiafya kutokana na hali ya mazigira na aina ya madini yanayochimbwa (tz. k. m. Ibid.: 109).

4. Muundo na mtindo

Mwandishi ametumia muundo rejeshi. Kila mara, bila ya kuwachosha wasomaji, amejitahidi kutumia mtindo wa kumweka fanani anayesimulia mambo mbele ya hadhira. Kwa mantiki hiyo, ameingizia nyimbo, muziki na mashairi ilimradi kuifanya hadhira yake iweze kushiriki kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano mwishoni mwa 'Kifungua Pazia' mwandishi anaitahadharisha hadhira yake (tz. ibid.: 12). Tunaweza kuyaona mashairi hapa na pale (tz. ibid.: 30; 48; 138; 215; 237; 277).

Upekee wa mtindo wake, licha ya kuwa na muundo rejeshi, ni ule ufundi wa pekee wa kumshirikisha msomaji katika usimulizi kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

> *Msomaji, nayaeleza haya wazi bila kukubabaisha kutokana na mshangao tulioupata.* (ibid.: 148)
>
> *Hebu turudi Dar es Salaam kuona kizaazaa ambacho Japhet Lupocho alikiacha huko.* (ibid.: 164)
>
> *Msomaji wangu, japokuwa nachelea kuharibu mtiririko wa masimulizi yangu kwa kutokukurudisha huko Rufiji, [...]* (ibid.: 177)
>
> *Ewe msomaji wangu, nahofia kwamba nitakuchosha bure kuyaelezea masimulizi yangu kwa undani.* (ibid.: 252)

Huo ni mtindo wa fasihi simulizi. Basi, kwa maneno mengine, Chachage amefaulu kuunganisha mbinu za fasihi simulizi na fasihi andishi katika riwaya hii.

Aina nyingine ya upekee imejidhihirisha katika uumbaji wahusika wa riwaya hii. Mathalani, majina ya wahusika yanaakisi tabia ya kila mmoja kwa kadiri ya matendo yake yaliyojitokeza katika mazingira mbalimbali tofauti. Amefaulu pia kukariri yale yanayonong'onwa na jamii kuhusu maslahi yao. Kwa upande mwingine ametumia wahusika walio hai na ambao matendo yao halisi yanaibuliwa kwa uwazi na kwa ukweli bila ya kuficha majina na vitendo vyao. Kwa mfano katika sura ya tano yanatajwa majina ya Bwana Millinga aliyeongoza Chama cha *Jumuiya ya Maendeleo ya Wananchi wa Ruvuma* katika vijiji saba na jinsi kilivyokuwa tishio kwa serikali hata kumfanya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Bwana Edward Barongo, akavivunja na mali zake zote zilinyang'anywa na polisi (tz. ibid.: 107).

4.1. Matumizi ya Lugha

Chachage S. L. Chachage ameandika riwaya hii *Makuadi wa Soko Huria* kwa Kiswahili sanifu na fasaha, kiasi kwamba maelezo ya fikra nzito na nyeti yametolewa kwa umbuji wa hali ya juu.

Hapa na pale ametumia lugha nyingine kama Kiingereza (tz. ibid.: 1; 5; 10; 14; 21; 48; 58; 71; 105; 124; 145; 179; 184; 188; 254; 276; 285; n. k.), na Kiarabu (tz. ibid.: 196; 197; 233; n. k.). Mara kadhaa ametumia Kiswahili chenye lahaja ya mahali husika, kwa mfano *"Sasi mimi kukaa hapa nyumbani kwangu* bwanji*?"* (ibid.: 36). Hii ni lahaja ya wakazi wa mwambao wa Ziwa Nyasa. Pia ametumia msamiati wa lugha za makabila mbalimbali. Mifano ni *mmbumba* [Kimpoto] likimaanisha mwanamke, *mhika* [Kimpoto] lenye maana ya mtu baki, mgeni asiye mzawa; *mkwavu* [Kimpoto] likimaanisha wavu; *myakaya* [Kingoni] aina fulani ya pombe za kienyeji; *mgowe* [Kibena] likimaanisha ufanyaji kazi kwa ushirika *kiyau* [ilivyoitwa na watu wa pwani].

Ametumia fani mbalimbali za kifasihi. Kwa mfano ametumia nahau, methali, misemo, misimu, tamathali za semi kadha wa kadha. Kwa kuimarisha utamu wa masimulizi yake ametumbukiza beti chache za mashairi hapa na pale (tz. kurasa 30; 48; 138; 194; 215; 237; 277). Ama hakika, kughani kwa mashairi au kuimba kwa nyimbo zenye muziki wa kuliwaza na kugusa hisia nzito huondoa machovu ya kumsikiliza fanani na masimulizi yake, lakini pia kunashirikishwa hadhira.

4.1.1. Methali

Mwandishi amekuwa hodari sana wa kutumia methali katika matukio muafaka. Mifano miwili ni:

Yaliyopita si ndwele, tugange yaliyopo na yajayo (ibid.: 11)

Uchungu wa mwana aujuaye mzazi au adhabu ya kaburi yaijua maiti! (ibid.: 200)

4.1.2. Tamathali za semi

Ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na kuipamba kazi ya sanaa ya kifasihi waandishi hutumia tamathali za semi zenye kuleta maboresho na utamu wa lugha. Mwandishi hakuwa nyuma katika kuzitumia baadhi ya tamathali hizo katika riwaya hii.

Tashihisi

Tamathali hii pia huitwa 'fasili ya binadamu', ambayo huipa vitu sifa au uwezo wa kibinadamu. Mfano mmoja ni *mmomonyoko kutafuna ardhi* (ibid.: 21).

Mubalagha

Hii ni tamathali ya usemi inayosisitizia hali ilivyo kwa mkazo wa neno lifungamanalo sawia na kile kinachoelezwa. Mfano mmoja ni *mieusi tii!* (ibid.: 39). Hapa *'tii!'* husisitiza juu ya weusi unaong'aa, yaani weusi kwelikweli. Kinyume chake tunasema *'mweupe pe!'*.

Tasifida

Tamathali hii ya usemi hutumika katika kupunguza au kuficha makali ya kauli au neno.

> *"Huko kwa Eliasi ndiko unakofanyia maasi yako ya kimwili?"* (ibid.: 63)

Kwa maneno ya moja kwa moja bila kuficha makali ingekuwa "Huko kwa Eliasi ndiko unakofanya ngono?" au "Huko ndiko mnakofanya vitendo vya zinai; uasherati; uzinzi; kujamiiana?"

Tashibiha / Mshabaha

Tamathali hii hutumika kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia viunganishi, kwa mfano *kama; mithili; mfano wa; kana kwamba,* na vinginevyo.

> *"Wewe unamkumbuka yule Oscar aliyetishia kunenepa kama kufutu?"* (ibid.: 71)
>
> *Ile furaha waliyokuwa nayo punde tu ikawa imeyeyuka kama samli juani.* (ibid.: 105)
>
> *[...] akiuangalia moshi wa sigara ile uliokuwa ukipanda juu mithili ya umbile la jini litokalo katika chupa ya kwenye hekaya za kale.* (ibid.: 132)

Dhihaka / Kejeli

Tamathali hii hubeza, hudharau, hubeua, huumbua, hukashifu, hufedhehesha, husuta, hukufuru, huponda, hulaumu na kulaani.

> [Mhusika Profesa wa Marekani:] *"Shirika la Fedha Duniani liliiambia Tanzania ibadili sera zake na kuruhusu masoko huria ndipo uchumi utaendelea, lakini yule kichwamaji Nyerere aligomea."* (ibid.: 87)
>
> [Mhusika Alibhai:] *"Ndiyo, nilikuwemo katika vile vikundi vya TANU, lakini mimi sikuamini hata mara moja kwamba maana ya Ujamaa ni watu wote kuwa maskini."* (ibid.: 119)

> [Mhusika Makoba:] *"[...] huyu padri. Yeye daima alikuwa na tabia moja. Kila aendapo kanisani kwa pikipiki yake alikuwa na tabia ya kusimama chini ya mwembe mmoja mkubwa sana na kukojoa pale kabla hajaendelea na safari yake. Hii [...] haikuwa tofauti kabisa na yule mnyama aitwaye fungo, ambaye, kila akiwa na haja huenda sehemu ile ile."* (ibid.: 137)
>
> [Mhusika Janga Mjuba akilewa chakari:] *"[...] nimehamia kwa Eliasi Mwasho toka juzi baada ya kuondoka nyumbani kwangu na kumwacha mke wangu aendelee kusali na sala zake, na haja zake za kimwili zikikidhiwa na Roho Mtakatifu."* (ibid.: 139)

Takriri

Takriri ni usemi unaorudiarudia neno, maneno, muundo, kauli, sentensi, au vipengele vingine.

> [Bibi yake mhusika Janga Mjuba:] *"[...] Elimu! Elimu si ufunguo wa maisha, bali ukombozi wenyewe. Ukasome kama Nyerere mpaka uwe kama Nyerere!"* (ibid.: 204)

Ni dhahiri kauli hizi pia zina udamisi na tashibiha.

Udamisi

Hii ni tamathali inayotilia chumvi kuhusu uwezo wa viumbe (wahusika) ili kuchekesha au kusisitiza jambo ambalo msanii hutumia ili kuisadifu hadhira yake.

> [Mhusika Janga Mjuba:] *"Ule mkutano ulikuwa ni fiksi kabisa, tena si fiksi tu, bali feki."* (ibid.: 27)
>
> [Bibi yake mhusika Janga Mjuba:] *"[...] Elimu! Elimu si ufunguo wa maisha, bali ukombozi wenyewe. Ukasome kama Nyerere mpaka uwe kama Nyerere!"* (ibid.: 204)

4.2. Migogoro

Katika riwaya hii kumezushwa migogoro mingi kuanzia ile ya mtu na nafsi yake, migogoro ya mapatena (wapendanao); migogoro katika familia; migogoro katika jamii; migogoro ya kitaifa na ya kimataifa. Baadhi ya migogoro imetolewa masuluhisho lakini mingi mingine haikutolewa suluhisho.

Mathalani, katika mgogoro wake binafsi Japhet Lupocho awali aliamua kujinyonga kwa kamba kule Rufiji, lakini anasalimishwa. Lakini baadaye Lupocho anauawa na walinzi wa Mooney.

> *Bwana Mooney aliingiliwa ofisini kwake na mfanyakazi wake wa siku nyingi na kuuawa kwa kukatwa na kisu. Walinzi waliposikia vilio, waliingia hima ofisini na kumshambulia Japhet Lupocho hadi akafa.* (ibid.: 286-287)

Mgogoro baina ya wanakijiji wa Nyamisati, Rufiji, na wawekezaji inatatuliwa na Wanarufiji wenyewe kwa hekima yao ya kurithi kutoka kwa mababu zao.

4.3. Upeo na Falsafa ya Mwandishi / Hitimisho

Kama alivyosema Profesa Shivji – ambaye kama tulivyoonyesha anatumika kama mmoja wa wahusika wa riwaya yenyewe – katika hotuba yake ya uzinduzi rasmi wa riwaya hii: Hii ni riwaya ya karne ya ishirini na moja ambayo ina makali huku na huko, pande zote mbili, kwani maudhui yake yanamkera kila mwananchi. Inaonyesha jinsi matukio ya kihistoria yalivyoathiri matarajio ya watu wa kawaida kuondokana na madhila.

> *"Chachage amekerwa na unyonge na dhuluma katika jamii yake, ameteswa na ukandamizwaji wa watu na amefarijika na ujasiri wa umma. […] Katika hili, yaani kuandika riwaya isiyokuza ushujaa wa mtu au watu binafsi, Chachage amemkaribia mwandishi wa kimapinduzi, Maxim Gorky. Kwangu mimi hii tu linanitosha kumweka Chachage katika orodha ya wasanii stadi wa Tanzania na wa bara la Afrika."* (Shivji 2000 [2002]: 94; 95)

Riwaya hii *Makuadi wa Soko Huria* ingeweza pia kulinganishwa na ile ya Kiingereza ijulikanayo kwa jina *The Roots* ya mwandishi Alex Haley kwa kadiri ya utafiti wa nasaba ya ukoo wa akina Lupocho. Kuna uhusiano ainaaina baina ya koo za Wanarufiji na wakazi wa ziwa Nyasa kwa upande moja na kwa upande wa pili hushabihiana na Wangoni, Wabena, Wahehe na Wazaramo. Ni riwaya inayosawiri maendeleo ya mwamko wa mwananchi kutoka wakati wa ukoloni, mapambano dhidi ya wakoloni hadi sasa.

> *Nyerere alipopita sehemu za Rufiji kwa mara ya kwanza mwaka huohuo* [1955]*, watu wa huko wakasema: "Kinjikitile* [sic] *amerudi kumalizia kazi ambayo aliianza!" […] "Hatutakuwa watumwa tena. Saa imewadia ya siafu kuwa pamoja na kumtoa nyoka pangoni!"* (Chachage 2002: 213)

Ni dhahiri kwamba watu wa kawaida wanajua mengi kwa vigezo mbalimbali mintarafu uwezo na upungufu wa viongozi wao wa nyanja mbalimbali. Mhusika Saada anamalizia hotuba yake bungeni kwa maneno yafuatayo:

> *"Tumekuwa tukifuatilia mwelekeo wa kisiasa na kiuchumi wa nchi yetu, nasi kama wazalendo tunahisi kuhainika. Kwa hiyo tukasema, sisi kama wapiga kura ni watu tunaotegemeana na Wabunge ambao ndio wawakilishi wetu halali. […] Wabunge na raia wanategemeana. […]"* (ibid.: 276)

Profesa ametumia kalamu yake ambayo inafanana na jambia lenye makali huku na huko. Jambia hilo laleta changamoto kwa wakiukaji maadili wote kujikosoa ili kuondoa shari inayoashiriwa na fukuto la mitanziko ya maisha ya kila siku ya jamii.

5. Marejeo

Chachage, Chachage Seithy L. 2002. *Makuadi wa Soko Huria.* Dar es Salaam: E & D Publishers Limited. 287 pp.

Shivji, Issa G. 2000 [2002]. Makuadi wa Soko Huria. *Mulika* 26. pp. 93-97 [Matini ya hotuba iliyotolewa kwenye uzinduzi rasmi wa riwaya tarehe 17/10/2002].